# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# CHUO CHA UALIMU BUSTANI

## UJENZI WA BWENI LA WASICHANA

## MKATABA WA UJENZI

### A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | MWAJIRI | MKUU WA CHUO<br>CHUO CHA UALIMU BUSTANI<br>S. L. P. 131 KONDOA<br>KNY:<br>KATIBU MKUU<br>WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA |
| 2 | JINA NA ANWANI YA FUNDI (*Mwajiriwa*) | Jina: ISAYA ERNEST LAIZER<br>Anwani: S.L.P 107 IRINGA<br>Simu: 0652-559977 |
| 3 | ENEO LA UJENZI | CHUO CHA UALIMU BUSTANI |
| 4 | MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI | KUJENGA JENGO LA BWENI LA WATU 80 KUANZIA MWANZO MPAKA KUKAMILIKA KWA AJILI YA MATUMIZI HUSIKA (KUFANYA KAZI ZOTE ZA UASHI, USEREMALA, UMEME NA BOMBA, KAMA ILIVYOONESHWA KWENYE JEDWALI LA KAZI) |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | **GHARAMA YA UFUNDI** *(+ Skills Development Levy 4.5% of work service)*: | **TSHS 26,300,400/=**<br><br>**SHILINGI MILIONI ISHIRINI NA SITA LAKI TATU NA MIA NNE TUU.** |
| 6 | **MUDA WA MKATABA**<br><br>(Tangu Kusainiwa kwa Mkataba): | Tarehe ya Kusaini. **27/01/2022**<br>Muda: **90 – SIKU**<br>Tarehe ya Kuanza Kazi. **27/01/2022**<br>Tarehe ya Kumaliza Kazi. **26/04/2022** |
| 7 | **MASHARTI YA MALIPO:** | • Hakuna Malipo ya Awali<br>• Fundi atalipwa kila baada ya sehemu ya kazi husika kukamilika, kukaguliwa na kuthibitishwa. |

**B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA**

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Mwajiri atatoa vitendea kazi vyote kama "concrete mixer", toroli, karai, ndoo, chepe, ngazi, n.k.
3. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
4. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na mafundi wote aliowaajiri na kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
7. Fundi atahusika na vitendo *(kama wizi, uharibifu wa mali za chuo)* vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
9. Ni marufuku Fundi au mafundi kuja kazini akiwa ametumia aina yoyote ya madawa ya kulevya, unywaji wa pombe na kuvuta bangi eneo la chuo. Ikibainika atachukuliwa hatua.
10. Mwaajiri hatahusika na malipo yoyote kwa mafundi wasaidizi na vibarua.

11. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika *(Retention Money)* na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.

12. Kiasi cha asilimia 4.5% kitakatwa na kuwasilishwa mamlaka ya mapato Tanzania (T.R.A) ikiwa ni kwa ajili ya SDL. (*Skills Development Levy 4.5% of workservice)*

13. Ucheleweshaji wa Kazi:

- Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

14. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri *(kutokana na fedha au vifaa)*, Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

15. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi kupigana au kuonesha viashiria vya aina yoyote ya kuhatarisha kuvunja amani katika eneo la kazi.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanachuo na hatua kali zitachukuliwa.

**MWAJIRI:**

Saini: ..........................

Jina: JOYNA ELISHA CHANAFI

SIMU: 0758-900881

Cheo: MKUU WA CHUO

Tarehe: **27/01/2022**

MKUU WA CHUO BUSTANI CHUO CHA UALIMU KONDOA

**FUNDI:**

Saini: ..........................

Jina: ISAYA ERNEST LAIZER

SIMU: 0652-559 977

Cheo: FUNDI MKUU

Tarehe: **27/01/2022**

ISAYA ERNEST LAIZER S.L.P. 107 IRINGA

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Saini: ..........................

Jina: DICKSON MSANGI

SIMU: 0784-523978

**SHAHIDI WA FUNDI**

Saini: ..........................

Jina: TOM MSENGI

SIMU: 0753-185006

Cheo: KAIMU MAKAMU MKUU WA CHUO

Tarehe: 27/01/2022

Cheo: FUNDI MSAIDIZI

Tarehe: 27/01/2022

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU BUSTANI**

**MALIPO YA FUNDI**

1. JINA LA MZABUNI: **ISAYA E. LAIZER**
2. KIASI ALICHOLIPWA **TSHS. TSHS. 26,300,400/=**